


NAME: .....

SCHOOL: ..... RANDOM NO: .....

**KISWAHILI**  
**Paper 1**  
**July/Aug. 2024**  
2 hours



# **AITEL JOINT MOCK EXAMINATIONS 2024.**

## **Uganda Certificate of Education**

**KISWAHILI,**

MUDA: 2:00hrs

### **MAAGIZO KWA WATAHINIWA.**

- Karatasi hii ina sehemu mbili: A na B
- Jibu maswali mawili kwa ujumla.
- Katika sehemu A, kuna maswali mawili. Chagua swali moja tu.
- Sehemu B ni ya lazima.
- Majibu yote yaandikwe kwenye karatasi uliyopewa.
- Swali la ziada halitasahishwa.

## SEHEMU: A

### UTUNZI WA INSHA

#### Ama

1. Kuanzia mwaka huu wa 2024, Jumuiya ya Afrika Mashariki inapanga kutumia Kiswahili kama lugha rasmi ya mawasiliano. Eleza jinsi wanainchi wa Uganda watafaidika na mpango huo.

#### AU

2. Mwandikie barua meneja wa kampuni ya simu za mikononi ya MTN kwa kupitia katibu mkuu ukimwomba kazi ya kufanya baada ya kumaliza masomo yako chuo kikuu cha makerere. Andika insha isiyo pungua maneno 120 wala 160.

### SEHEMU.B

*Soma hotuba kisha uifupishe kwa maneno yasiyozidi sitini(60) ukionyesha mambo muhimu yaliyosemwa na mgeni Mkuu.*

Mheshimiwa makamu wa Mkuu wa chuo, Waheshimiwa Mabalazi na Mawaziri, wenyekiti wa kongamano la “Kiswahili 2000”, waheshimiwa viongozi wa vyama na serikali, Maprofesa, Wahadhiri, na watoa makala katika Kongamano hili, washiriki wa kongamano, Wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana.

Awali ya yote, sina budi kutoa shukrani zangu za dhati kwa waandalizi wa kongamano hili kwa Mwaliko wa kuwa Mgeni Rasmi katika Sherehe hii ya ufunguzi. Kwangu mimi ni heshimu kubwa kushirikishwa katika mjadala unaohusu uendelezaji wa lugha ya Kiswahili ambayo ni lugha rasmi ya pili ya Taifa la Uganda.

Kwa heshima, napenda kuwakaribisha nchini Uganda wageni wetu nyote mliotokaa nje ya nchi. Kufika kwenu kushiriki katika kongamano hili ni ushahidi kuwa mnazienzi na kuzithamini juhudi zinazofanywa na wanauganda, kupitia kwenye vyombo vyao vyao vya kukuza, kujenga na kuendeleza lugha na utamaduni wa Mwafrika. Aidha, ni ushahidi kuwa mnaithamini lugha ya Kiswahili na kutambua umuhimu wake katika kujenga umoja, uelewano na mshikamano wa waafrika wa ukanda huu wa bara letu.

Bila shaka kukubali kwenu kushiriki katika semina hii ni dalili nzuri yenye kudhihirisha kuwa mko tayari kushirikiana nasi kuyatekeleza malengo ya kukuza na kuendeleza lugha

ya Kiswahili , na luhgha zetu za kiafrika kwa jumla ili ziendeele kuwa utambulisho wa Mwafrika popote popote pale alipo.

Ntaka vilevile nichukue fursa hii kuipongeza kwa dhati kabisa taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili (TUKI) kutoka Tanzania kwa kazi kubwa na muhimu inayofanya katika kukiendeleza na kukikuza Kiswahili. Mwaka juzi, tulisheshereheke miaka sabini ya uhai wa TUKI, ikiwa ni ushahidi wa kutosha kwamba taasisi hii inatoa na inaendelea kutoa mchango Mkubwa katiak kukikuza na kukiendelea Kiswahili. Miaka sabini si kipindi kifupi kwa taasisi; nafikiri hakuna taasisi mbalimbali zilizotangulia hapa Afrika Mashariki kwa jumla. Napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza wote, walio hai na waliotangulia mbele ya haki, kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kutekeleza majukumu ya TUKI hata ikadumu hadi leo. Nakishukuru na kukipongeza chuo kikuu cha Dar es salaam kwa kuiongoza na kuilea taasisi hii muhimu tangu Mwaka 1964.

MWISHO